

**WRITERS SPEAK  
ESSAYS ON LITERATURE  
AND DEMOCRACY**

**Edited with an Introduction**

**By:  
KITULA KING'EI  
AND  
HENRY INDANGASI**

Published by: **Writers Association of Kenya**  
C/O Department of Literature  
University of Nairobi  
P.O. Box 30197 Nairobi.

First Published 1997  
© Writers Association of Kenya

All rights reserved. No part of this book may be reproduced in any form without the written permission of Writers' Association of Kenya.

Typeset & Printed by: J. I. Katuku Enterprises  
P.O. Box 75341  
Nairobi.

## ACKNOWLEDGMENTS

The Writers' Association of Kenya wishes to acknowledge the financial and moral support of the United States Agency for International Development which has made it possible for us to publish this book. In particular, we thank Mrs. Nancy Gitau of that agency for her warmth and encouragement.

We also want to thank the administrative and secretarial staff of the University of Nairobi's Department of Literature, to which we are affiliated, for providing the required basic services.

Lastly, we want to thank all our members for keeping the Association alive. Special thanks go to those who participated in the workshops in which we brainstormed on the nature and function of the literary and critical essay.

CONTENTS

INTRODUCTION

*By Henry Indangasi*

Page

i

DEMOCRACY: PERSONAL REFLECTIONS

*By Wanjira Muthoni*

1

\* CREATIVE LITERATURE, DEMOCRACY AND GOOD GOVERNANCE

*By Kitula King'ei*

7

TOWARDS A DEMOCRATIC SOCIETY: THE AFRICAN EXPERIENCE

*By Humphrey O.D. Webuye*

15

CULTURAL DIVERSITY & NATIONHOOD: IMPLICATIONS FOR DEMOCRACY

*By Arthur I. Luvai*

20

DEMOCRACY: THE MIRAGE WOMEN MUST SWIM IN

*By Helen Oronga Mwanzi*

26

IN THE COMPANY OF DEMOCRATS

*By Henry Indangasi*

31

FREEDOM OF CHOICE: KENYAN WOMEN WRITERS

*By Sophie W. Macharia*

41

CREATIVE LITERATURE AND DEMOCRACY IN AFRICA

*By Ciarunji Chesaina Swinimer*

48

LUGHA, MWANDISHI NA KUVUMILIANA

*By Richard M. Wafula*

61

THE SEARCH FOR TRUE DEMOCRACY IN KENYA

*By Lumumba Esese and Egara Kabaji*

68

DEMOCRACY FOR THE FEW: EXAMPLES FROM THE BUKUSU COMMUNITY

*By Monica Mweseli*

76

FLAVOURING DEMOCRACY WITH KISWAHILI

*By Mwendwa Mbatia*

84

THE ROMANCE OF NATIONHOOD: KENYA AS WORD AND DESIRE

*By Peter Amuka*

89

## LUGHA, MWANDISHI NA KUVUMILIANA

*R. M. Wafula*

Dhima ya lugha katika shughuli ya kueneza maoni na imani za mtu ni muhimu. Bila kuwepo na lugha, itakuwa vigumu kuwasiliana kusemezana na kuambiana kwa lengo la kuwajenga walimwengu angalau wenye shabaha na nia ya kujizatiti kufahamu na mitafaruku yao wenyewe.

Wakimdongoa mwanafalsafa Bertrand Russell, Fromkin na Rodman wameelezea kwamba:

Hata mbwa akibweka kwa  
ufasaha mkubwa vipi, hawezi  
kukuambia kwamba wazazi walikuwa maskini na waminifu  
(1978:39)

Maelezo haya yanaeleza umuhimu wa lugha katika mawasiliano ya jamii. Pia, yanatuonyesha upekee wa lugha kama chombo cha kuwasiliana au kinachomwezesha mtu kusema analotaka kwa namna anavyotaka au anavyotarajia kueleweka.

Demokrasia inahusu kusemezana na kuelewana katika misingi inayoridhisha malengo na maadili ya walio wengi. Karatasi hii inakusudia kuonyesha kwamba ikiwa masuala yanayohusu utumiaji wa lugha hayatashirikishwa na juhudi za wanajamii wa maeneo hayo kutokana na ufinyu wa aina yoyote, hatuna budi kwamba juhudi hizo zitaishilia kuwa mjanggo.

Swali ambalo pengine msomaji anapaswa kujiuliza ni vipi lugha inavyoweza kutumiwa kufanikisha malengo ya kujenga jamii ambamo wanachama wake wanaheshimiana na kuvumiliana, yenye mapendeleo machache, jamii ambayo inakadiria kuzingatia kwamba licha ya tofauti hata ya watu wawili, wanaweza kujiundia kigezo madhubuti, kikawa 'kisingizio' maalumu cha kuwapa sababu ya kuishi? Swali hili limezushwa katika muktadha mpana. Swali lingine linalohusiana nalo; Je, lugha ni chombo muhimu cha kuwaunganisha watu na kuwaelekeza katika njia za kuheshimiana na

kujenga jamii ya kidemokrasia?

Ikiwa jibu kwa swali hili ni ndiyo, basi bila shaka jibu hili limekita katika misingi ya lugha. Sababu ni kwamba kuna mkondo wa fikra za wataalamu wanaoamini kwamba lugha kila mara husheheni mielekeo, mitazamo na imani za mtumiaji wake. Umuhimu wa lugha umo katika dhima ya kuelezea ishara zinazowasilisha maana tofauti tofauti. Kwa kifupi, lugha inaweza kutumiwa kwa shari au kwa heri kulingana na ishara za maana zinazonasibishwa au zinazohusishwa nayo. Ni katika sifa hii ya lugha ambapo tunapata ama uwezo wa kujenga au wa kubomoa na kuporomosha.

Baadhi ya waandishi, kwa mfano, wamerejea hali ya Tanzania na kudai kwamba lugha inaweza kuwaauni watu kufikiliza madhumuni yao ya kibinafsi na ya kitaifa. Nakisia ya kwamba huenda waitifaki wa maoni haya wakasema kuwa katika majira haya ya mabadiliko, hali kama ya Tanzania ambapo lugha moja ya taifa hutumiwa inaweza kufadhilisha uweleano na uvumilivu kuliko hali ambamo lugha tofauti huongewa.

Kwa upande mwingine kunayo mataifa mengine ambako kunazungumzwa lugha moja au mbili tu, hata hivyo, hali nyingine kama ukoo, utabaka au tofauti zilizoletwa na ukoloni zimesabababisha chuki na kuzusha hali inayokanganya na kutatiza uelewano. Hali hii inadhihirisha kwamba lugha pekee haiwezi kuzalisha utengamano.

Kutokana na miktadha inayokinzana kuhusu matokeo ya matumizi ya lugha katika jamii zinazojibitisha kuimarisha demokrasia, inaonekana kwamba swala la lugha na mahusiano yake na dhana ya demokrasia kama inavyojaribiwa linapaswa kuangaliwa kwa jicho penyezi zaidi. Lapaswa kuangaliwa hivyo kwa sababu kama ilivyobainika kitambo kidogo kilichopita, kuna athari nyingi zinazoingiliana na kuvurugana na dhima ya lugha, zikadhalilisha uwezo wa lugha wa kupigania malengo ya kiutu.

Kwa maoni yangu, lugha inaweza kutumiwa na Wakenya kuwasilisha tajriba zao, hisi zao na fikra zao kuhusu vipera tofauti tofauti vya demokrasia kama vinavyothibitika katika maisha yao. Lakini ili lugha itimize wajibu huu itahitaji kurutubishwa na mitazamo ya kijamii inayohimiza kuheshimiana na kuvumiliana. Jambo hili litawezeshwa na maandishi yanayowafundisha watu ukweli kuhusu majirani zao badala ya

kueneza uvumi usiokuwa na msingi. Lugha ni mithili ya udongo ulimaji ambao waweza kufinyanga chombo chochote. Ni juu ya mfinyanzi kuunda chombo kinachowafaidi wanajamii wengi zaidi.

Katika miaka ya sitini na ya sabini shabaha kuu ya waandishi ilikuwa kupigana heshima ya utamaduni wa Mwafrika. Waandishi wa wakati huo walifikiria kwamba licha ya wao kuelekishwa kupitia katika lugha za mkoloni, lugha zilezile zingetumiwa kama vyombo vya ukombozi, vyombo vya kulazimisha ulimwengu wa mkoloni kukaa kichwa mgomba. Haya ndiyo maoni yanayosomwa na kuhisiwa katika kurasa za wanasanaa kama Ngugi wa Thiong'o na Chinua Achebe. Hata maandishi yanayohusu utamaduni wa Mwafrika kama *Naushangilia Mlima Kenya* yamepewa msukumo wa kutungwa na imani hii.

Katika miaka ya themanini, mwandishi mashuhuri zaidi nchini Kenya amepondekea upande wa kujieleza katika lugha yake ya kwanza. Amefanya hivyo kwa imani kwamba matumizi ya lugha inayoeleweka na lugha-jamii fulani ndiyo itakayowafaidi watumiaji wanaohusika. Mbali na mtazamo huu wa kimapinduzi, waandishi wengi wameendelea kuandika katika lugha ya kiingereza. Idadi nzuri ya waandishi kama Mkangi, G. K. King'ei, Y. M. Kingala, Z.A. Burhani na Rocha Chimera wanaandika kwa Kiswahili.

Matumizi ya lugha ya kwanza, kiswahili na kingereza kwa ujumla yanawakilisha hali ya lugha isiyokwepeka nchini. Ni hali inayoweza kuwasaidia wanajamii kuelewa majukumu yao mbalimbali kutangamana na viwango vyao vya utumiaji wa lugha. Ni kweli isiyopingika kwamba jamii yetu ni mseto wa watu wanaozungumza lugha nyingi na tofauti na wenye kudhibiti viwango aina vya usomi. Ndiposa hali hii katika matumizi ya lugha imetokea.

Naam, maoni yangu ni kwamba mwandishi anaweza kutumia lugha yoyote ile maalumu inazungumzwa humu nchini na maadamu ina kusudi la kuhimiza sera zinazojenga na kuimarisha demokrasia. Demokrasia ni dhana kongwe, ni dhana ambayo tunaizungumzia pasi kufahamu vipengele vyote vya majukumu yanayoandamana nayo. Kwa sababu maana nyingi zimehusishwa na demokrasia, dhana hii imekuwa tata na kanganyifu. Hivyo, inajuzu kuiangalia, kuikagua na kuichuja upya lugha inayotumika katika tungo zetu.

Hali ya binadamu aghalabu hushurutisha watu kutenda na kujenga mitazamo kulingana na mazingira yaliyowazunguka. Mageuzi ya mazingira hulazimisha kuwepo kwa mabadiliko ya mambo ambayo pengine hapo awali yalichukuliwa vingine. Tungo zetu zinazohusu maswala ya kisiasa zinapasa kutumia lugha inayoainisha na kuzungumzia upungufu na pia kuzungumzia mafanikio ya pote jingine. Demokrasia ni uvumilivu ni ukadirifu, na kwa mwandishi hii inamaanisha matumizi ya lugha wastani. Ni utaratibu wa kuishi ulio na masharti yanayohusiana na haki na wajibu kwa wale wanaoukubali. Bila kujitolea utaratibu huu wa maisha hauwezi kuuona mwanga wa kesho.

Sera inayotazamia kumwongoza mwandishi anayezungumzia demokrasia sasa itatofautiana kwa kiasi fulani na mtazamo uliomuelekeza mtunzi wa miaka ya sitini na ya sabini, na hata baadhi ya mitazamo iliyoratibisha tungo za miaka ya themanini. Mwandishi wa wakati wetu inafaa ajiulize swali ambalo Jean Paul Sarte alijiuliza takribani miaka hamsini iliyopita ijapokuwa jibu lake si sharti lisadifu lile la Sartre. Swali lenyewe ni, mwandishi humwandikia nani?

Ili kukadiri kwa mapana ugumu wa swali hili, inahitaji kujifikirisha juu ya hali halisi ya uwezo wa kusoma na kuandika katika mazungumzo yetu. Jamaa wengi katika maeneo yetu ndio wanaelekea kujua kusoma na kuandika. Ni wazi kwamba demokrasia kama utaratibu wa kutawala imekubaliwa katika eneo letu shingo upande. Hakuna kujitolea kwa hali na mali kwa upande wa wale wanaoshika hatamu za uongozi kuimarisha huu utaratibu. Tawala nyingi zinastahimili kuwaona watu waziouliza kwa kutojua kuliko wale waliozinduka na wenye kusaili kila wanapokabiliwa na hali inayotatanisha.

Ikiwa jamaa wengi hawajui kusoma na kuandika inaelekea kwamba wamehamasishwa kufikiria juu demokrasia na tajriba zao wenyewe. Kimbunga cha kimataifa kilichoyeyusha mgawanyiko wa ulimwengu katika mirengo iliyokinzana kiliwakuta watu waliojiandaa kujadili kiitikadi juu ya demokrasia.

Ingawa sina tarakimu za kutegemewa, nafikiria kutokana na mazingira yangu kwamba lugha za kwanza na lugha ya kiswahili zimekuwa vyombo vya uzindushi zaidi kuliko lugha ya kiingereza. Kauli hii inampa

mwandishi majukumu mawili. Moja ni kuwa mwandishi anatarajiwa kuandika maandishi yanayofikika na watu zaidi. Kufanya hivyo kutaafikiana na dhamira na mwito wa wakati wetu. Pili mwandishi atakuwa chombo mwafaka cha kuipa hekima jamii yake iwapo atainisha viwango vya usomi vya wanajamii na kuandika tungo zinazofungamana na viwango vile. Ijapokuwa sifa muhimu ya demokrasia ni kustahimiliana, sioni kwa nini maadili yake yasifundishwe kwa kujitolea kama dini za kikristo zilivyofundishwa zilipoingizwa hapo mwanzoni barani Afrika. Mielekeo ya kidemokrasia, kwa mfano, inaweza kunyunyizwa katika hadithi za watoto na wasomi wa ngumbaru.

Katika muktadha wa dini, nakumbuka vitabu kama *Safari ya Msafiri* vilivyotumiwa kwafunzia wale waliohitimu kiwango cha kimsingi cha kusoma na kuandika. Kutokana na kazi hizi vipa imara zaidi vilipeanwa na kushindiliwa; ndivyo nilionavyo jukumu la mwandishi anayepaanwa mada ya demokrasia ikiwa hataki kukengeuka mathalan mwenzake aliyetunga katika miaka ya sitini na ya sabini.

Ukweli ni kwamba mwandishi wa miongo ile alijizungumzia mwenyewe kuliko alivyoihadhira jamii iliyomzunguka. Aliandika kuhusu ukoloni na athari mbaya za utamaduni wa kigeni. Lakini huu ulikuwa mjadala nafsi ya uliokusudia kuililia nafsi yake mwenyewe. Nafsi iliyogawika kutokana na migogoro ya kitamaduni na nafsi iliyokosa utengano na mazingira yake. Mwandishi anayezungumzia demokrasia katika mwongo huu anaweza kujiopoa na hali hii kwa kuzingatia mahitaji ya wale anaowandikia, na pia kwa kutilia maanani uwezo wao wa kukabiliana na maandishi yake. Anaweza kukuza ufahamu wa wasomaji kama ambavyo masuala penyezi ya mafundisho ya kidini yanavyoenezwa kupitia katika maandishi yanayosomeka na kufahamika kwa urahisi. Pamoja na kutumia lugha inayokuza mitazamo ya kuvumiliana, mwandishi pia ana wajibu wa kutumia lugha inayohimiza haki na usawa wa jinsia mbalimbali. Akiligusia swala hili katika utangulizi wa diwani ya *Kina cha Maisha*, marehemu Kadenge Kazungu amesema:

Kwa kuendelea kumsifu mwanamke

Kwa sifa kama: mwenye shingo

ya upanga, mwendo wa maringo

ama kwa kumfananisha na ndege au tunda kwa kusudi la kusifia uzuri wake tu, kumepotosha na kuugubika ukweli wa maisha wanayoishi wanawake wengi katika jamii nyingi za kiswahili na za Kiafrika kwa ujumla. Kumeendeleza ile dhana kwamba wanawake ni viumbe wa kutazamwa na kustajabiwa kwa uzuri wao tu na wala sio kama binadamu wanaostahiki haki sawa na wanaume au hata na wanawake wengi wao (uk. viii)

Semi, methali, tashibih, jazanda na matamshi mengineyo yanayodhalilisha haki na heshima ya baadhi ya wanajamii yanapaswa kufanyiwa ukaguzi na kurekebishwa.

Hadithi zinazosawiri ukatili, maonevu zimetanda kotekote. Kwa hakika ukatili na maonevu yamekuwepo tangu mtu alipoanza kuitawala sayari hii. Kinachosemwa ni kwamba hadithi zilizokolea wahusika wakatili na waovu kama majitu zitatusaidiaje kuvua majoho ya uajabu ambayo baadhi ya watu wamejivisha na kuyatumia kuwakandamiza wanajamii wengine? Tanzania ni kwamba masimulizi haya mara nyingi huwa yamekusudiwa wasomaji ambao hawajakomaa kiumri na kimaarifa.

Lugha ya kitamathali haikosolewi hapa. Inavyosemwa ni kwamba itazingatia hali halisi ya wasomaji wako.

Hatimaye, demokrasia haimaanishi kwamba wote wanaofuata kanuni zake wataridhika nusu bini nusu. Kuna hatari ya wachache kuwa madhulumu wa maongozi yanayojifikiria kukidhi haja za kila mtu. Ili nao wajihusishe na na mkondo wa kiutu unaoongoza, baadhi ya haki zao zinaweza kufikiwa. Ebrahim Hussein katika tamthilia ya Mashetani ameandika kuhusu Cowboy mmoja anayewaangamiza wahindi wekundu wengi. Usifikirie kwamba yule mchungaji ni mmoja. Anawakilisha fikra za wengi zaidi kuliko wahindi wekundu wanaotimuliwa.

Lugha ina dhima muhimu ya kukuza utaratibu wa kukosoana kwa

kuvumiliana, ya kutuwezesha kutumia msamiati mkadirifu na wastani unaoafikiana maisha ya kiutu. Lugha hiyo ndiyo itakayoelezea matumaini yetu ya kisiasa na kiuchumi. Sioni maana nyingine ya demokrasia kwa wakati huu.

### Marejeleo

- |                          |                                    |
|--------------------------|------------------------------------|
| Bunyan, John (1980)      | <u>Safari ya Msafiri</u>           |
| Mwanza:                  | Inland press.                      |
| Burhani, Z.A. (1987)     | <u>Mwisho wa Kosa</u>              |
|                          | Nairobi: Longman                   |
| Hussein, E.N. (1971)     | <u>Mashetani</u>                   |
|                          | Nairobi: Oxford University press   |
| Kenyatta, Jomo (1971)    | <u>Facing Mount Kenya</u>          |
|                          | Nairobi: Heinemann                 |
| Kingala, Y.M (1984)      | <u>Anasa</u>                       |
|                          | Nairobi: HEB                       |
| Mkangi, G.K. (1984)      | <u>Mafuta</u>                      |
|                          | Nairobi: HEB                       |
| (1995)                   | <u>Walenisi</u>                    |
|                          | Nairobi: EAEP                      |
| Mohamed, S.A (1985)      | <u>Kina cha Maisha</u>             |
|                          | Nairobi: Longman                   |
| Ngugi wa Thiong'o (1981) | <u>Writers in Politics</u>         |
|                          | Nairobi: Heinemann                 |
| (1986)                   | <u>Decolonising the Mind</u>       |
|                          | Nairobi: Heinemann                 |
| Rodman & from kin (1978) | <u>An introduction to Language</u> |
|                          | New york: Holt, Rinehart & Winston |
| Sartre, J.P. (1950)      | <u>What is Literature?</u>         |
|                          | London: Methuen & Company          |